MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 11 TOLEO 41

JUNI 5, 2009

KIJARIDA CHA BURE— TOA NAKALA 2 NA GAWA BURE!

KASHFA YAFUKUTA

RA KUVULIWA URAIA?



Mbunge wa Igunga Bw. Rostam Aziz

Na. Mwandishi Maalum

Mbunge wa Igunga na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi ambaye pia ni mfanyabiashara maarufu nchini Bw. Rostam Aziz anaweza akajikuta katika matata mengine kabisa endapo atashindwa kuthibitisha uraia wake wa Tanzania kufuatia tetesi ambazo zimekuwa zikizagaa tangu mara ya kwanza alipoibuka katika siasa za Tanzania mwaka 1994 kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Igunga Bw. Charles Kabeho.

Baada ya kifo cha Kabeho CCM ilimteua kijana ambaye hana historia ndani ya Chama Cha Mapinduzi kuziba pengo hilo. Kijana huyo alitambulishwa kwa wananchi kuwa ni "Rostam Aziz" na ya kuwa familia yake ina 'historia' ndefu hapo Igunga na kuwa baba yake alikuwa ni mfanyabiashara wa mchele wilayani humo. Umaarufu wa mzee huyo ulitosha kabisa kufanya watu waamini na kumkubali Rostam.

Hata hivyo siyo wote waliloonesha kukubali jambo hilo na mi-nong'ono ikaanza chini kwa chini ikihoji juu ya historia ya Rostam. Baadhi ya watu walikana kujua uwepo wa "Rostam" huyo Kwa wengine alijulikana kama mwana familia aliyekuja kutoka Uajemi (Iran) na kuishi na familia hiyo kutokana na undugu wa karibu ingawa siyo ule wa mtoto na mzazi.

Tetesi hizo zilipozidi kuliandaliwa wazee kadhaa wa huko Igunga (chanzo kimoja kinataja idadi ya wazee sita) ambao (Inaendelea Uk. 2)



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!**

Ndani ya Toleo Hili

RA kuvuliwa uraia	1,2, 3
Mshirika wa RA aula!	1,4
RA kuvuliwa Uraia?	3
Da Jessy na Ndoa	4
Riwaya ya Mwanakijiji	5
Maoni ya Mhariri	5
Picha, Katuni na Maoni	6

...UTEUZI WA NONI: JK KACHEMSHA?

Na. Rashid Mahmoud

Katika hali ya kushangaza na isiyotarajiwa japo kuwa inayoeleweka Rais Kikwete amemtua aliyekuwa Afisa wa Benki Kuu wakati wa wizi wa fedha za EPA Bw. Peter Efraim Mayunga Noni kuwa Mkurugenzi mpya wa Benki ya Raslimali (TIB) .

Wakati wizi wa Fedha za EPA unatokea Bw. Noni ndiye alikuwa Mkuu wa Kurugenzi ya Sera za Uchumi, ambayo chini yake ndiyo idara ya kusimamia Akaunti ya Malimbikizo ya Madeni ya Nje (EPA) ilikuwepo.

Uteuzi huo umefanyika wakati ambapo Bw. Noni ni shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka katika kesi inayowakabili watu waliokuwa chini yake ambao kwa mujibu wa ushahidi wake mwenyewe Mahakamani walikuwa wanapitisha nyaraka zote za kughushui mikononi mwake (Inaendelea Uk. 4)

RA KUVULIWA URAIA?

walijitokeza hadharani (kwenye moja ya mikutano) na kudai kuwa wao wanamfahamu Rostam na ya kuwa ni kweli ni "mtoto" au mwanafamilia ya Aziz. Kwa muda mjadala ulifungwa kule Igunga na Rostam akaenda na kuchaguliwa kuwa Mbunge akiwa kijana wa miaka 25 hivi (kama tarehe yake ya kuzaliwa kwenye tovuti ya Bunge ni sahihi).

Baada ya kuingia Bungeni Rostam ndani ya miaka michache aliibuka kuwa mbunge mwenye nguvu kiasi cha kuweza kuwa Meneja wa Kampeni ya Urais wa mgombea wa CCM Bw. Jakaya Kikwete na pia kuwa Mweka Hazina wa Chama cha Mapinduzi. Gazeti moja la kimataifa lilifikia mahali pa kumtaja kuwa Rostam ni "King Maker" wa Tanzania, yaani mtu ambaye kwa uwezo wake anaweza kupachika viongozi hata wale wa ngazi za juu kabisa.

Katika muda wote wa miaka zaidi ya 15 ambayo Rostam amekuwa Mbunge wa Igunga amepanda chati za kisiasa nchini hadi kufikia kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na mara baada ya Rais Kikwete kupata Urais kuna watu walikuwa na mashaka kuwa angeweza kuukwaa Uwaziri wa aina fulani. Hata hivyo baadhi ya vigogo wa CCM walipinga uwezekano huo kutokana na kujua historia iliyo nyuma ya Rostam na cheo cha Uwaziri kingevutia udadisi usiokaribishwa.

Katika maisha yake ya kibiashara Rostam amejulikana zaidi katika kile kinachoaminika ni umiliki wa biashara mbalimbali na hisa katika makampuni mbalimbali na hivyo kumfanya miongoni mwa watu mashuhuri nchini. Pamoja na ukweli huo, uchunguzi unaonesha ni makampuni machache sana ambayo yanabeba jina lake moja kwa moja wakati mengi kati yao yakiwa na majina aidha ya ndugu zake au watu mbalimbali kiasi kwamba ni vigumu kumhusisha na makampuni mbalimbali ambayo kwa nje yanajulikana ni ya kwake.

Hata hivyo, tetesi juu ya uraia wake hazijakoma toka mwaka 1994. Kumekuwepo na watu huko Igunga na sehemu nyingine ambao wamekuwa wakihoji historia ya Rostam ambayo imekuwa ni ya kificho na hadi hivi sasa hakuna mtu yeyote ambaye ameweza kujitokeza kwa mamlaka ya kuaminika kuthibitisha kuwa kweli Rostam ni Mtanzania.

Baadhi ya wabunge ambao ni wakongwe ndani ya CCM waliozungumza na mwandishi huyu wiki chache zilizopita wamekiri kutokuwa kulisikia jina la Rostam ndani ya CCM kabla ya 1994 na wapo ambao wamekiri kuwa wanafahamu wazi kuwa Wazazi wa Rostam wapo Iran na ni raia wa Iran na hawajawahi kuwa Raia wa Tanzania wakati wowote.

"Unajua uraia wa Tanzania siyo kama wa Marekani, unaweza ukazaliwa Tanzania na usiwe raia wa Tanzania (ukiondoa wanadiplomasia wa kigeni wanaoishi Tanzania)" amesema Mbunge mmoja wa CCM ambaye ni mwanasheria. Akifafanua Mbunge huyo ambaye hakutaka kutajwa jina lake kutokana na unyeti wa mada yenyewe alisema kuwa "Uraia wa Tanzania unakuja aidha kutokana na kuzaliwa na wazazi ambao ni Watanzania au kwa kuomba uraia na zaidi ya yote kwa kuukana uraia wa kigeni wa wazazi wa mtu".

Mbunge huyo alitolea mfano wa watu mbalimbali ambao wamewahi kuvuliwa uraia wao ingawa walizaliwa Tanzania na kwa muda mrefu walijulikana kuwa ni raia wa Tanzania. Miongoni mwa mifano ambayo inatumiwa hata katika masomo ya uraia katika nchi mbalimbali ni kuvuliwa uraia kwa Jenerali Ulimwengu ambaye amewahi kuwa Mbunge na Mkuu wa Wilaya akijitambua na kutambulika kuwa ni raia wa Tanzania na kada mzuri wa Chama cha Mapinduzi.

"Watu wengi waliomfahamu Jenerali waliumizwa sana na jambo lile kwani wengi waliishi na kumtambua kuwa ni Mtanzania mzalendo hivyo kuvuliwa kwake uraia kwa sababu wazazi wake ilidaiwa hawakuwa wa Tanzania na yeye hakuwahi kuukana uraia huo wa wazazi wake alipofikisha miaka 18 kulishtua watu wengi" alisema Mbunge huyo.

Kwa mujibu wa Mbunge huyo endapo Rostam atavuliwa Uraia wake kwa sababu kama za Jenerali basi hilo halitakuwa jambo geni nchini na itaonesha kuwa kweli sheria ni msumeno. "Sheria ni kipofu na haiangalii hadhi, jina, umaarufu, utajiri au nafasi ya kisiasa ya mtu " alidai mbunge huyo. Hakuna ushahidi kama RA amewahi kuomba uraia wa Tanzania au kuukana wa wazazi wake.

Historia ya maisha ya Rostam ina utata mkubwa na kwa muda mrefu siyo yeye wala uongozi wa chama chake ambao umewahi kutoa majibu yanayojitosheleza na yenye ushahidi wa kisayansi kuthibitisha kuwa Rostam ni raia wa Tanzania.

Baadhi ya maswali hayo ni hilo la uraia wa wazazi wake (siyo 'ndugu'), elimu yake ya awali (msingi na sekondari) na pia suala la elimu ya Juu. Katika tovuti ya Bunge Rostam ametajwa kuwa ni mhitimu wa elimu ya Uchumi na gazeti la East African Business lilisema mwaka 2006 kuwa ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza. Hata hivyo uchunguzi wa mwandishi wa makala hii umefuatilia Chuoni hapo na Mtanzania aitwaye Rostam Aziz haonekani kuwa ni mhitimu hapo. Hata hivyo, mbunge mwingine aliye karibu na Rostam ambaye alizungumza na mwandishi siku chache zilizopita alidai kuwa kwa ufahamu wake Rostam ni mhitimu wa London School of Economics.

Juhudi za kumpata Katibu wa Bunge Dr. Kashilillah hazikufanikiwa ili kutolea maelezo juu ya wasifu wa Rostam. Vilevile jitihada za kumtafuta Rostam mwenyewe kutoa maelezo zilishindikana baada ya simu yake kuita kwa muda mrefu bila kupokelewa.

Zaidi ya utata wa uraia wake, utata mwingine upo kwenye jina lake. Jina lake hasa la kisheria ni nani. Kwa muda mrefu amekuwa akijulikana kama Rostam Abdurasul Aziz. Hata hivyo, katika rekodi mbalimbali za kabla ya mwaka 1994 mtu ambaye anahusishwa na familia ya Bw. Aziz "Mchelee" alijulikana kwa jina la Rustam A. Chakaar. Baada ya mwaka huo mtu anayejulikana kama Rostam Aziz ametokea akibadili jina na kuacha kabisa kutumia jina la "Chakaar" kama ndugu zake wengine wanavyotumia hadi hii leo.

Haijulikani ni lini Rustam alibadili jina lake la kisheria na kuanza kutumia jina la Rostam Aziz na zipo tetesi kuwa yawezekana kabisa mtu aitwaye Rustam na yule ambaye anajulikana kama Rostam leo hii si mtu mmoja. Utata huo wa majina unaongezwa zaidi baada ya kugundulika katika mojawapo ya makampuni ya "Rostam" majina ya watu watano ambao inadaiwa ni tofauti yametumika na uchunguzi wa kina umeonesha watu hao hawapo Tanzania na hawajawahi hata mara moja kujulikana Tanzania na hivyo

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

ROSTAM KUVULIWA URAIA?

kuonesha kuwa kuna ulaghai uliofanyika kwa makusudi.

Hadi hivi sasa hakuna mwandishi au chombo cha habari huru na ambacho kimethubutu kuhoji juu ya historia ya maisha ya Rostam na kumtaka ajibu maswali hayo ambayo kwa mtu wa kawaida si magumu hata kidogo.

"Maswali haya yanastahili kujibiwa, lakini ni mtu mmoja tu ambaye ana majibu yake naye ni Rostam" amedokeza Mhariri wa gazeti moja maarufu nchini ambaye naye pia alikataa kutaja jina lake kwani gazeti lake linadaiwa kumilikiwa na Rostam. "Hata mimi ukiniuliza sijui historia yake, zaidi ya kile ambacho watu wengine wanakijua kwa juu juu" amesema mhariri huyo ambaye amewahi kuwa mahiri katika hoja za kupinga ufisadi hadi pale alipojikuta ni muajiriwa wa mojawapo ya makampuni ya Rostam.

Kwa mujibu wa Mhariri huyo, maswali hayo hayawezi na hayastahili kujibiwa na chombo chochote cha serikali au CCM au uongozi wa vijana wa mkoa fulani. Haya ni maswali ambayo Rostam pekee ndiye mwenye uwezo wa kuyajibu kwa uwazi na kwa ukweli na kutoa majibu yenye kuridhisha.

Hata hivyo, uchunguzi unaonesha kuwa kwa muda mrefu vyombo mbalimbali vya serikali haviko tayari kufanya uchunguzi juu ya Rostam kwani endapo ukweli utajulikana unaweza kukitikisa chama na nchi. Hii inadaiwa pia ndiyo ilikuwa sababu ya kumzuia Rostam kuzungumza Bungeni kwenye suala la Richmond kwani baadhi ya hoja ambazo zingeweza kutolewa na timu ya kina Mwakyembe katika kile kinachodaiwa "kujibu mapigo" kinahusu moja kwa moja historia ya Rostam ambayo wabunge wengi tu ndani ya CCM wanaifahamu kwa undani na ingeweza kufungua kile kinachoitwa kama "kisanduku cha Pandora" ambaye kwenye hadithi za kale za Kigiriki alikatazwa kufungua lakini kwa udadisi wake alipofungua kisanduku hicho ndio alifungulia maovu yote tunayoyaona duniani leo hii na hakukuwa na njia ya kuyarudisha kwenye kisanduku hicho.

"Bw. Mwandishi, hili siyo suala la kulifuatilia kwa undani kwani linawagusa watu wakubwa na watu wengi sana ambao wamejitahidi kwa muda mrefu kuzima mjadala wa maisha ya Rostam kwani endapo ukweli wote utafunuka itakuwa ni aibu kubwa kwa nchi na kwa chama na ninakuomba sana usiliendeleze hili kwani utakachofungua hutoweza kukirudisha" alitoa ushauri mmoja wa viongozi wakongwe wa CCM ambaye pia ni mbunge wa muda mrefu na mjumbe wa mojawapo ya vikao vyake vya juu.

Hata hivyo, baadhi ya wasomi wanaamini kuwa kama kweli serikali inafuata utawala wa sheria kama ambavyo imekuwa ikidai basi haina budi kuhakikisha kuwa mjadala wa Uraia na maisha ya Rostam ambaye ni miongoni mwa watu wenye nguvu kubwa nchi unamalizwa kwa kuweka taarifa wazi za historia yake ambayo inaweza kuthibitishwa na mchunguzi yeyote huru.

"Binafsi ningependa Bunge litoe tamko juu ya uraia na ustahili wa Rostam kuwa Mbunge wa Igunga kwa kulieleza taifa wasifu wa Rostam hata kama yeye mwenyewe hatokuwa tayari kutoa majibu ya maswali hayo na kama Bunge halina majibu basi limsimamishe Ubunge hadi majibu hayo yatakapotolewa na kutosheleza" alisema Mbunge mwingine mwanamama ambaye amejipatia umaarufu kwa kuwa na msimamo huru Bungeni.

Hata hivyo, kutokana na ukaribu wa Rostam na maraia Kikwete pamoja na Mkapa na jinsi alivyoshiriki katika kukisaidia Chama cha Mapinduzi na wabunge mbalimbali uwezekano wa uchunguzi huru kufanyika haupo.

Hilo linatokana na ukweli kuwa hadi ameweza kufikia hapo alipofikia inasemwa kuwa Rostam ameweza kuwaweka katika "anga zake" viongozi mbalimbali akiwasaidia katika harakati mbalimbali za kibiashara na hasa jinsi ya kufungua makampuni hewa au kuwekeza fedha nje ya nchi ikiwemo huko Costa Rica, Cayman Islands, Isle of Man na Falme za Kiarabu ambako ana urafiki wa karibu na baadhi ya watawala wa falme hizo ambao miongoni mwao ni wale waliouziwa utajiri wa hifadhi ya Loliondo mwaka 1992 na wakarudi tena kupitia kampuni ya Dowans Tanzania Limited.

Zaidi ya yote, kuanguka kwa Rostam kama kutatokea kutokana sababu hiyo ya uraia kutasababisha kashfa kubwa ya Uraia na usalama wa Taifa pale ambapo mtu ambaye si raia ameweza kushiriki katika kampeni za urais, kupanga safu ya viongozi mbalimbali na hata kuweza kupata mahusiano ya karibu na viongozi wa usalama wa taifa.

"Bw. Mwandishi, usiwe na shaka, watu wa usalama wa taifa wanafahamu kabisa juu ya ukweli wa suala la uraia wa Rostam lakini wao kama wanasiasa walio juu yao hawana ubavu wa kufunua ukweli huu na hivyo kimsingi mstari wetu wa kwanza wa kinga (first line of defense) umeshavunjwa" amesema mbunge mwingine wa upinzani ambaye pamoja na wenzake wanatarajia kuibua hoja nzito kwenye kikao cha Bunge wiki chache zijazo.

"Ndiyo maana sisi wengine tangu mwaka jana tumeendelea kupiga kelele juu ya Idara yetu ya Usalama wa Taifa kwamba imekuwa 'compromised' na hivyo bila mabadiliko ya ndani na ya makusudi usalama wa nchi yetu bado uko matatani" alisema kwa kujiamini.

Kwa mujibu wa watu wa karibu na Rostam, Mbunge huyo tangia mwaka jana ameanza kuona dalili za mambo yake "kumuendelea vibaya" na ameanza taratibu kuhamisha uwekezaji wake toka nchini na kwenda nchi za nje ambako huko kinyume na Tanzania anatumia majina yake katika kufungua biashara au kufanya biashara. Mojawapo ya mambo yanayotajwa ni mfano wa hilo ni kusudio lake la kutaka kuhamisha hisa alizonazo kwenye kampuni ya Vodacom jambo ambalo limekutana na upinzani kutoka kwa wasimamizi wa sekta ya Mawasiliano.

Ukiondoa huko Vodacom, Rostam ameanza kupanua mbawa zake kwa kuingia katika uwekezaji katika nchi za Afrika ya Kusini na inasadikika pia kuingia huko Kenya na hata Rwanda. Kwa mujibu wa mipango hiyo endapo kweli Rostam ataanguka kama inavyotarajiwa kutokana na uzito wa kashfa mbalimbali zinazomzunguka basi hatopata hasara kubwa ya kifedha kwani makampuni mengi yanayotajwa kuwa ni ya "yake" hajaweka jina lake na pale ambapo anajua kuna jina lake ameanza kupunguza uwekezaji wake kujiandaa kwa zali lililoko mbele yake.

Soma bure

PETER NONI APANDISHWA CHEO NA KIKWETE

kabla ya kumfikia aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu marehemu Daud Ballali.

Bw. Noni ambaye pamoja na mkewe ni wamiliki wa kampuni ya Planetel ambayo ilikuwa na hisa katika kampuni ya Vodacom kabla hajaziuza hisa hizo kwa kampuni inayosadikiwa kuwa ni ya Mbunge wa Igunga Bw. Rostam Aziz (CCM) ya Mirambo.

Baada ya kushindwa kuzuia wizi wa EPA kutokea ambao ulipoteza karibu zaidi ya shilingi bilioni 133 Bw. Noni alipewa idara mpya ndani ya Benki hiyo ambapo alizawadiwa cheo cha Ukurugenzi wa Idara ya Mipango na Mikakati ya Benki Kuu hadi hivi sasa anbapo ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Raslimali.

Katika ushahidi wake mahakamani mapema mwaka huu Bw. Noni alielezea jinsi ambavyo malipo ya EPA yalikuwa yakifanyika na maelezo yake mengi yanaonesha kumbebeshea lawama Gavana Ballali kwani hayaambatani na ushahidi wowote wa kimaandishi isipokuwa maneno yake yeye Noni kuwa Ballali "alisema" au "aliagiza".
Katika sehemu mojawapo ya ushahidi huo mbele ya Hakimu Lyamunga Bw. Noni alikiri kuwa idara ambayo ilikuwa inapitia madai ya madeni hayo ambayo washtakiwa Anna Komu, Rajab Maranda, Imani Mwakosya na Bosco Kimela walikuwa wakiifanyia kazi ilikuwa chini yake.

Bw. Noni alikiri pia kuwa hakuwa anapendezwa na utaratibu wa ulipaji wa madeni hayo kwa mtindo uliopendekezwa na Ballali na kuwa alimshauri Ballali kubadilisha mtindo huo, ingawa Ballali inadaiwa hakumsikiliza.

Hata hivyo, Bw. Noni alikiri kuwa ushauri wake huo wa jambo zito na nyeti ambalo lingeweza kuokoa fedha nyingi aliufanya kwa mdomo na si kwa maandishi na hivyo kumfanya shahidi pekee wa mazungumzo hayo kwani mtu anayedaiwa kumuambia (Ballali) alishafariki na hivyo hawezi kubisha au kujitetea.

" ni kweli nilikuwa na nia hiyo, lakini nilimweleza gavana katika mazungumzo, lakini sikuwa nimeweka nia hiyo kwa maandishi." alikiri katika mahakama ya Kisutu katika ushahidi wake.

Zaidi ya yote mmoja wa wanasheria wa kampuni Malegesi Law Chambers Bhyidinka Michael Sanze ndiye ametajwa kuwa ni wakili aliyetia sahihi nyaraka mbalimbali za makampuni hayo yaliyokuwa yakidai fedha za EPA.

Ni wakili huyo huyo ambaye aliandika hati ya kiapo (Affidavit) kwa kamati ya Rais ya kuchunguza EPA amedai kuwa kati ya watu waliokuwepo wakati makubaliano ya Kagoda na Benki Kuu yanafanyika (yaliyoipa Kagoda kama shilingi bilioni 40 za EPA) ni Bw. Peter Noni.

Wengine ambao amewataja katika makubaliano hayo ni Gavana Ballali, Rostam Aziz, na aliyekuwa Rais Bw. Benjamin Mkapa.

Pamoja na uzito wa tuhuma zinazomzunguka Bw. Noni, Rais Kikwete ameamua kumpa nafasi nyingine kwenye Benki muhimu bila kutoa nafasi ya uchunguzi wa kuhusika kwake kwenye EPA.

Haieleweki ni kwa kigezo gani mtu aliyeshindwa wajibu wake BoT anapewa nafasi nyingine TIB wakati sakata zima la EPA ndio bado kabisa limeanza na halijafikia tamati.

DA:JESSY— KUJIANDAA KWA NDOA— 3

Na. Jessica Fundi



Unapoamua kufunga ndoa na mtu mojawapo ya vitu vikubwa kabisa ambavyo huna budi kuvikubali na kuvikumbatia ni kuwa umeamua kujitangaza hadharani kuwa kuanzia wakati huo tamaa yako, hamu yako, na mapenzi yako yatakuwa kwa yule mwenzako wa ndoa.

Kimsingi ndoa inahalalisha na kubariki tamaa za mwili kwa mwenzi wako. Nje ya ndoa watu huwakiana tamaa na kutamaniana kingono na wapo ambao huzitekeleza tamaa hizo kwa huzuni zao wenyewe baadaye. Hata hivyo mwelekeo huo wakati mwingine husababisha hisia ya hatia (guilty feelings) hasa kwa wale ambao wamelelewa katika maadili ya kidini au kijamii ambayo yanatukuza ndoa.

Na pale ambapo mahusiano yanakoma kwa sababu yoyote ile (kutoelewana, kuchukiana n.k) basi mtu anaachana na mpenzi wa awali na kutafuta mwingine na kuendeleza vitendo vya ngono ambavyo hujikuta ni vya starehe ya miili zaidi kuliko furaha ya moyo na utulivu wa akili.

Na hata pale ambapo watu wanaamini wako "pamoja" hali halisi ni kuwa hawako pamoja. Kilichopo ni kuwa wao wawili wamekubali kushirikishana miili yao bila ya kushirikishana maisha yao yote, njozi zao, hofu zao, n.k Walichotengeneza hasa ni "ushirika wa ngono".

Hata hivyo, ndoa inabadilisha hayo yote. Licha kuunganisha nafsi mbili, ndoa huunganisha "miili". Hii ina maana ya kwamba mimi kama mke ninayo haki ya kumtamani mume wangu, saa yoyote, na wakati wowote bila kujisikia vibaya.

Ninakuwa na haki na mwili wa mwenzangu na yeye anakuwa na haki na mwili wangu. Na katika miaka ya mwanzo ya ndoa haki hii inatakiwa kutekelezwa kwa furaha yote. Mume wangu anaponitaka hata kama wakati mwingine najisikia nimechoka na nina mambo "kichwani" inanipasa kumkubalia kumpa kilicho "haki yake".

Ndio maana mimi si muumini mzuri wa "kumnyima" mume wangu unyumba kwa sababu ya maneno tuliyorushiana au kuwa kaniudhi kwenye jambo fulani. Nilitangaza hadharani kuwa "nimekubali kumchukua".

Kukubali huku ni msingi mkubwa wa furaha katika ndoa na mahusiano ya baadaye. Hata hivyo, ndoa siyo masuala ya ngono tu ni mambo mengine pia. Kujiandaa kwa hili la tendo (kwa usahihi) la ndoa na mwenzi wako na kuwa ni yeye pekee, ni mwanzo tu.
Niandikie: **dajessy@klhnews.com**

Soma Bure
hoja zenye nguvu

ALTARE YA MACHOZI

"Vivian Tembo, unampokea Charles Mugisha kuwa mume wako wa ndoa, umuenzi na kumtunza, kumpenda na kumlinda katika shida na raha, katika magonjwa na afya mpaka kifo kiwatenganishe?" Padre Amedeus Minja alimuuliza bibi harusi.

"Ndio nampokea!" Vivian alijibu kwa sauti ya upole, lakini iliyonaswa vilivyo na vipasa sauti vya Kanisa la Mtakatifu Joseph Jijini Dar-es-Saalam. Jibu lake hilo lilisababisha mlipuko wa vigelege, hoi hoi, na makofi ambao nusura uziangushe kuta za Kanisa hilo maarufu. Kabla ya chereko chereko hizo kukoma kwaya ya Mtakatifu Joseph iliyokuwa ikiongozwa na Veronica Mwangwi ilirukia na kuanza kuimba kibwagizo chao maarufu cha "Nimekuchagua wewe, kati ya wanaume wote, uwe msaidizi wangu!" Mara kibwagizo hicho kilipoisha, Padre Minja alimgeukia kijana Mugisha na kumrushia swali hilo hilo.

"Charles Mugisha, unampokea Vivian Tembo kuwa mke wako wa ndoa, umuenzi na kumtunza, kumpenda na kumlinda, katika shida na raha, katika magonjwa na afya mpaka kifo kiwatenganishe? Aliuliza huku akielekeza kinasa sauti upande wa Charles.

Charles alijaribu kufungua mdomo wake na kutoa jibu la "ndio nampokea"; mdomo haukufunguka. Alijihisi kupatwa na kizungu zungu cha ghafla huku miguu ikimtetemeka kama mianzi ikipigwa na upepo. Alijaribu tena kutamka maneno hayo ya kukubali lakini ulimi wake uligandamana na kaakaa la kinywa chake kama umetiwa gundi ya mbao. Koo lilimkauka na moyo wake ulianza kumwenda mbio huku mdundo wake ukisikika kwa mbali kwenye vipasa sauti vya kanisa hilo. Ukimya mkubwa ulitanda kama ukimya wa kaburi. Hakupiga mtu chafya, wala kujaribu kupigwa mwayo. Wazazi wa bibi harusi, wanawali waliofuatana na bibi harusi wote walikodoa macho kumwelekea Charles, na macho yakawatoka utadhani gololi! Kila mtu alijiuliza ni kitu gani kimemsibu kijana huyo.

Kanisa lilikuwa kimya wakati Charles anatafuta maneno ya kujibu. Padre Minja akaona ajaribu tena kumuuliza kijana huyo aliyevalia suti ya kupendeza ya rangi nyeusi ambayo koti lake lilikuwa na michirizi ya kumetameta ya rangi ya maziwa na kingo zake zikifika hadi magotini. Upande wa kushoto alikuwa amening'iniza ua jekundu la waridi, na miguuni akiwa ametinga viatu vya Armani ambavyo alizawadiwa na rafiki yake toka Italia.

"Charles Mugisha, unampokea Vivian Tembo kuwa mke wako wa ndoa, umuenzi na kumtunza, kumpenda na kumlinda, katika shida na raha, katika magonjwa na afya mpaka kifo kiwatenganishe?" Alirudia tena Padre Minja.

Ndani ya moyo wake na akili zake Charles alikuwa kama birika la chai ambalo lilikuwa likichemsha maji yakachemka na yakiwa tayari kumwagika kutokana na nguvu za msukumo wa joto lake. Alikuwa karibu kupasuka kwa msukumo wa hofu, woga, aibu, hatia, na kila aina ya hisia hasi. Alijaribu kukohoa kidogo kusafisha koo lake. Alimwangalia bibi harusi ambaye wakati huo mdomo wake ulikuwa umebakia wazi kiasi cha kuwa kama mlango unaokaribisha inzi! Charles alimuangalia Vivian na akajaribu tena kutoa kauli ya kukubali. Haikutoka. Alikuwa kama gari lililozima katikati ya reli huku treni likija kwa kasi toka upande mmoja na jitihada zote za kuliwasha zikishindikana.

Vivian aliinua macho yake na kuyagonganisha na ya mchumba wake, mawazoni alikuwa na maswali milioni moja na moja ambayo angependa kumuuliza kimemsibu kitu gani. Alipomuangalia vizuri aligundua kuwa Charles alikuwa amelengwa na machozi na yeye mwenyewe Vivian alijigundua kuwa machozi yameanza kufurika kwenye macho yake na kuanza kufanya michirizi kwenye pande za mashavu yake huku yakiharibu poda, wanja, na vimetameta alivyokuwa amepambwa navyo kwa ajili ya harusi hiyo. Wapenzi hao wawili walijikuta wakibubujikwa na machozi.

Charles alimgeukia Padre Minja na kumwashiria amsogelee ili amnong'oneze kitu.

"Baba Padre, naweza kujibu swali hilo, lakini kabla sijafanya hivyo naomba nafasi ya kuungama kitu kwako na kwa Vivian, tafadhali" Alisema kwa sauti ya upole, ya chini lakini iliyokuwa na uhakika wa kile isemacho. Padre Minja alitingisha kichwa kuashiria amemuelewa. Vivian hakujua Charles amemnong'oneza kitu gani padre huyo, maswali akilini mwake yaliongezeka na kuwa milioni moja na mbili. Padre Minja aliwageukia waumini ambao wote walikuwa kimya wakisubiri kwa hamu kujua ni nini kinaendelea. Waliokuwa wambeya hawakuchelewa kuanza kuzusha uvumi, na wenye simu wakaanza kutumiana ujumbe kuwa Vivian kaachwa altareni!

"Wapendwa katika Bwana!" Padre Minja alianza kuzungumza kwa sauti kakamavu iliyomgutusha kila mtu kanisani humo. "Tumesikia jibu la bibi harusi, lakini bwana harusi kabla ya kutoa jibu lake, ameniomba twende chemba ili afanya maungamo ya dhati kabla kutoa jibu hilo. **(Itaendelea)**

TUNATAFUTA WAANDISHI

Kijarida cha Cheche za Fikra kinatafuta waandishi wa kujitolea kuandika makala mbalimbali na kutuma habari kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania kwa ajili ya kijarida hiki na pia kwa toleo la mtandao.

Kwa yeyote ambaye angependa kushirikiana nasi atuandikie na mada ambazo angependa kuwa anaandikia (mwandishi wa makala atakuwa na sehemu yake kwenye tovuti yetu)

Tuma: **mhariri@klhnews.com**

MAONI YA MHARIRI: TEUZI HIZI NI AIBU!

Katikati ya tuhuma dhidi ya Zombe na mauaji ya wale wafanyabiashara watatu, IGP akamteua kuwa Mkuu wa Polisi wa Rukwa; katikati ya tuhuma za kashfa yaAlex Stewart, Rais Kikwete akamteua Basil Mramba kuwa Waziri; Katikati ya tuhuma za ufisadi wa Rada, Rais Kikwete akamteua Andrew Chenge kuwa Waziri (tena mara mbili) na Chama chake kumteua kwenye kamati ya maadili! Hii ni amini usiamini!

Sasa hivi katikati ya kesi za EPA, na hata hatujui baadhi ya wahusika wake wote (hususan suala la Kagoda) mmoja wa maafisa waliohusika na mikataba hiyo ya makampuni feki na ambaye anakiri kuwa kiunganishi kati ya Gavana na ofisi ya madeni (wanakotoka washtakiwa) Rais Kikwete amemteua mtu huyo kuwa Mkuu wa Benki ya Rasilimali.

Tunashindwa kuelewa kama kuna utaratibu wowote wa kuchunguza wateuliwa mbalimbali (vetting process). Kama upo au haupo, dalili zote zinaonesha kuwa tunaburuzana tu. Hii ni aibu!

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha ya Wiki



Mwenyekiti wa TLP Bw. Agustine L. Mrema akiwa amezungukwa na vijana wajasiriamali.


PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KATUNI ZA WIKI





KUTOKA KWENYE MTANDAO

1. Kufuatana na taarifa za Noni mwenyewe, nyaraka za (kugushi) zilikuwa zinapelekwa kwa Gavana Balali, kisha zinapitia kweke naye anazipeleka kwa Mwakosya. Zikisha shughulikiwa zinarudi kwake kisha anazipeleka kwa Gavana kisha zinalipwa. Sasa inakuwaje Gavana na Mwakosya wanatiwa hatiani wakati yeye mtu wa kati anapandishwa cheo?

2. Kuhusu experience, kila Banker anafundishwa namna ya ku detect fraud. Sasa ilikuwaje external auditors kwa muda mfupi tu waone makosa kobao ya documents fake zilizo tumika wakati Noni alikuwa na muda mrefu zaidi kuzikagua. halafu si document moja tu bali kibao.

3. Wizi wa Shs. 133 Bil umefanyika chini ya macho yake. Utetezi wake eti alimtahadharisha Gavana kwa MDOMO. Jee huyu anajua hata utaratibu wa kazi?

Jee hivi hii TIB itapona kweli? - **TK**

Mtu anayeshuhudia wizi ukifanyika, na ana uwezo wa kuzuia wizi huo au kwa namna fulani ananufaika na wizi huo huyo ni sehemu ya wizi. Peter Noni ni mnufaika wa wizi wa EPA.. anatakiwa awe miongoni mwa wanaotiwa pingu lakini kwa vile ni amekuwa mbia wa mastermind wa EPA anachofanya ni kuzawadiwa.—**Mwanakijiji**

mtafute mfanyakazi yeyote wa BOT akupe wasifu wa huyu jamaa ndio utajua jamaa yupo kwenye kundi gani,NONI hakuwa na uwezo wa kuzuia ule wizi,na kwa kushuhudia kwake ndio maana leo hii ni shahidi wa serikali na naweza kukwambia kuwa NONI si mnufaika wa EPA.—**Mtimti**

Mafisadi wote wanasema wamefuata maagizo toka juu. Kama hajaiba basi tusimchafue lakini kama alishuhudia wizi na hakusema kitu, huyo ni mwizi tu.—**Mtanzania**

Umeshasahau juzi kuhusu uteuzi wa wakuu wa wilaya walioteuliwa wakiwa na kesi za rushwa mahakamani na mmoja alikuwa chini ya uchunguzi wa TAKUKURU? - **Mazingira**

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*